Gazeti la kwanza la Islam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Enyi mlioamini, si halali kwenu kuwarithi wanawake kwa nguvu; wala msiwazuie (kuolewa) ili mpate kuwanyang'anya baadhi ya vile mlivyowapa, isipokuwa wawe wamefanya uovu ulio wazi; na kaeni nao kwa wema ; na kama mkiwachukia, basi huenda mchukie kitu na AllahAmetia heri nyingi ndani yake. (An-Nisaa 4:20)

JUZU 82 No. 237 | SHABAN-RAMAZ.1444AH | MACHI 2023 | ZAHOOR 1402 HS | BEI TSH. 700/=

Mwongozo Mkuu, Manufaa na Fadhila

zisizo na Mwisho za Qur'ani Tukufu kwa Mtazamo wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu

Ubora wa Qur'ani Tukufu - Muhuri wa Vitabu

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah al-Fatiha, Khalifa mtukufu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) alisema kwamba alipokuwa akitaja baraka za Qur'ani Tukufu, Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba baraka zake ziko bayana kabisa, kama ilivyokuwa wakati wa Mtukufu Mtume (saw).

Kuhifadhiwa kwa Milele Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) aliyesema kwamba ingawa Waislamu wengi wameipuuza Qur'ani Tukufu, nuru yake, baraka na athari zake ziko hai na nzuri na Mwenyezi Mungu ameendelea kutuma watu kuihifadhi na kuilinda Qur'ani Tukufu; kama Anavyoahidi: *"Hakika Sisi Tumeyateremsha mawaidha haya na hakika Sisi ndio Tuyalindao". (Qur'ani Tukufu, 15:10)*.



Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tanoatba akihutubia waaminio Ijumaa katika Masjid Mubarak, Uingereza Tarehe 03 Februari, 2022. Akieleza Mwongozo Mkuu, Faida na Fadhila zisizo na Mwisho za Quran Tukufu kwa Mtazamo wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba katika zama hizi, Mwenyezi Mungu amemtuma mtumishi wa kweli wa Mtukufu Mtume (saw) ili kuhifadhi na kuieneza Qur'ani Tukufu kote ulimwenguni. Inasikitisha kwamba tangu mwanzo wa ujio wake, wale watu wengi waliwasilisha picha katika wanajamaat nchini, kwani wanaojiita wanazuoni na maulama wamefanya ni kusudio lao kumpinga Masihi Aliyeahidiwa (as) na kutengeneza vizuizi katika njia yake ya kuieneza Qur'ani Tukufu. Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa hivyo ndivyo ilivyo hasa nchini Pakistani, ambako maulama huzua matatizo na wanaweza kupata uungwaji mkono wa baadhi ya wanasiasa wasiotafuta chochote zaidi ya umaarufu. Wanabakia katika majaribio ya kuendelea ya kutoa mashtaka ya uwongo ya kufuru dhidi ya Waahmadiyya. Khalifa mtukufu (atba) aliomba kwa ajili ya uhuru wa wale ambao kwa sasa wamefungwa kimakosa. Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa ujio wa Masihi Aliyeahidiwa (as) na mafundisho yake yamedhihirisha hazina na maana nzuri za Qur'ani Tukufu na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya inafanya kazi ya kue-

Endelea Uk wa 3..

Ahmadiyya Yakutana na Rais wa Zanzibar Dr. Hussein Ally Mwinyi

Na.
Sheikh Shaban A. Shunda

Waswahili husema penye nia pana njia, na pia husema safari moja huanzisha nyingine, na huu ni uzoefu wa wazi katika maisha ya wanadamu kwenye Nyanja zote, pindi anapoanza kulifanyia kazi wazo Fulani, basi hupata njia ya kutanua wazo hilo na wakati mwingine na wasidizi wa kulifanya hilo hujitokeza. Na wakati mwingine wazo la mwanzo laweza kuwa lilikuwa katika kipimo kidogo lakini matokeo ya mwisho yakaonekana kuwa wazo lilikuwa kubwa sana. Mnamo mwisho wa mwaka 2022 ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Ahmadiyya Tanzania ulikutana na Mhe. Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania Dk. Samia Suluhu Hassan huko Zanzibar. Baada ya kumalizika kwa mkutano huo ambao ulikuwa chanzo cha furaha na muamko za mkutano huo katika mitandao yao ya kijamii na kutoa maoni yanayoonyesha fahari yao katika tukio lile. Hivyo basi baada ya kuisha mkutano ule Naibu Amiri Maulana Abid Mahmood Bhutt Sahib alishauri kuwa ni vyema tufanye mipango ya kumuona na Rais wa Zanzibar, na maandalizi yalinza kufanyika wakati ule ule, na jukumu hilo alikabidhiwa Rais wa Mkoa wa Kijamaat Zanzibar bwana Saidi Mbwana, naye alilibeba kwa shauku na kutokana na mazingira yake ya kujichumia kipato au naweza sema ajira halikuwa jambo gumu sana kwake kwani ilimchukua wiki moja au mbili kukamilisha jukumu hilo, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Taratibu zote zilifuatwa kwa upande wa makao makuu na kukakamilishwa ndipo Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya Tanzania ilipokea mwaliko kutoka Ikulu rasmi.



Picha ya pamoja ya Raisi wa Zanzibar akipokea Zawadi ya Kurani Tukufu na Mwakilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya, Amir na Mbashiri Mkuu Maulana Sh. Tahir Mahmood Chaudhry siku ya matembezi mjini Unguja.

Siku iliyopangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa kihistoria ilikuwa ni Jumamosi tarehe 4 mwezi wa 2, 2023, Amiri na Mbashiri Mkuu Tanzania Maulana Tahir Mahmood Chaudhry Sahib aliandaa safu yake ambayo angeambatana

Endelea Uk wa 4..

Mwendelezo Hutuba ya Huzur ya 03.02.2023 uk. 12..

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Uchuro wa Jinsia Moja

Ni maradhi mengi waliyo tuachia wakoloni lakini mawili yanafurutuada yetu tusipo angalia maana nzima ya uhuru wetu itapotea kama bado haijapotea.

Mkoloni alipoweka mguu wake Afrika hatua ya kwanza aliyo ichukua ni kuhakikisha kuwa amedhalilisha, amebeza kila kitu kinacho husu utamaduni, desturi ya mila zetu. Hakuna njia nyingine ya kumtawala binadamu hadi kwanza umuaminishe kuwa yeye si chochote si lolote na busara yake ni kufuta kabisa utu wake. Na kama Dodoki kufyonza kila kitu anachokiamini nakukiabudu Mtawala. Hata kama kitu chako ni kizuri kiasi gani hicho kiweke pembeni kwani ni sehemu ya shetani. Tulikutwa na ndoa zetu za wake wengi na tukaambiwa pia hiyo nayo ni njia ya shetani. Toka wakati huo tumekuwa kama Mtumishi wa Fataki Kagoro, ambaye kila alicho kisema Fataki Kagoro yeye daima aliitikia *'Inya waitu'* Ndio bwana. hata kama mvua inanyesha, Fataki Kagoro akisema jua linawaka mtumishi wake atadakia na *'Inya waitu'*. Bara la Afrika tumekuwa watu wa *Inya waitu*. Uchafu wowote unaotokea kwa walio tutawala sisi sauti yetu ni moja *Inya waitu*. Mtu aliye na uhuru ambaye Allah amemjalia akili na busara anawezaje kuendelea kusema *inya waitu?* Ni maafa na masikitiko makubwa. Ni giza wakati wajua kali!

Waafrika tuna mila na desturi zetu, kama sisi wenyewe hatuwezi kuziheshimu ataziheshimu nani? Kwa kasi kubwa tena ya kutisha mbegu ya kile kinachoitwa mapenzi ya jinsia moja, kinapandwa katika Afrika kwa hakika hayo si mapenzi ya jinsia moja isipokuwa ni uchuro wa jinsia moja. Zuzu ana bwata kwenye kundi la watu anasema ni kundi kama kundi jingine.

Wakati wa Baridi kali akisema ni baridi kama jamaa zetu wanapokuwa na jaribio lao wanakwenda taratibu kwa hila kutetea. Wanazungumza ni haki za binadamu. Ni ua la Walid ambalo ndani yake kunanyoka. Wanazungumzia haki za faragha. watetezi hawa walikuwa wapi wakati watu weusi walipo uzwa kama Dagaa? Walikuwa wapi wakati makaburu walipo kuwa wanawatesa ndugu zetu wa Afrika kusini?

Kama Afrika tutaungana kupigania uhuru. Kuna ulazima wakukusanya nguvu za pamoja kupambana na janga la uchuro wa jinsia moja. Wanatakiwa wanaolipenda bara hili wasimame kuiambia Dunia kuwa huo ni mwiko kwetu. Inatakiwa waseme hili wana Siasa, wasomi kwa kauli moja walaani balaa hili lakini maneno tu hayawezi kusaidia kitu kwani maneno matupu hayavunji mfupa, jukumu la kwanza liko kwa wazazi. Wewe mzazi unaonesha hasira kwa balaa hili? Unalaani na kukemea hapo nyumbani? unafuatilia mwenendo wa mwanao magazeti anayo soma, vitabu anavyosoma mitandao? Tunaelewa ni kazi ngumu kinacho takiwa ni kutimiza wajibu wako na walimu wanayo nafasi nzuri ya kupambana na janga hili wanakaa na watoto kwa muda mrefu. Wakikemea jambo wanafunzi watawasikiliza Waalimu wanaathari kubwa kwa wanafunzi. Nani asiyejua kuwa wanafunzi huiga sauti hata mwendo wa awali? Waalimu ni askari na mstari wa mbele katika vita hii. Viongozi wa Dini wanao wajibu wakulinda hekalu la bwana wawe mstari wa mbele katika vita hii. Waandishi wa habari wana uwezo mkubwa wa kubadili upepo wa jamii watumie Kalamu zao kuinusuru Afrika. Anayepinga balaa hili hapati msaada hawa wa Afrika wamekwenda mbali sasa wanatutishia kutumia Silaha ya msaada. Tusipo jikomboa kutoka kwenye mnyororo wa msaada kuna hatari ya kuuza uhuru wetu kwa thamani ya kalila!



QUR'AN TUKUFU

وَلُوْطًا اِذْ قَالَ لِقَوْمِهٖۤ اَتَاْتُوْنَ الْفَاحِشَةَ
مَا سَبَقَكُمْ بِهَا مِنْ اَحَدٍ مِّنَ الْعٰلَمِيْنَ ﴿۸۱﴾

اِنَّكُمْ لَتَاْتُوْنَ الرِّجَالَ شَهْوَةً مِّنْ دُوْنِ
النِّسَآءِ ؕ بَلْ اَنْتُمْ قَوْمٌ مُّسْرِفُوْنَ ﴿۸۲﴾

وَمَا كَانَ جَوَابَ قَوْمِهٖۤ اِلَّاۤ اَنْ قَالُوْۤا
اَخْرِجُوْهُمْ مِّنْ قَرْيَتِكُمْ ۚ اِنَّهُمْ اُنَاسٌ
يَّتَطَهَّرُوْنَ ﴿۸۳﴾
فَاَنْجَيْنٰهُ وَاَهْلَهٗۤ اِلَّا امْرَاَتَهٗ ۖ كَانَتْ مِنَ
الْغٰبِرِيْنَ ﴿۸۴﴾

وَاَمْطَرْنَا عَلَيْهِمْ مَّطَرًا ؕ فَانْظُرْ كَيْفَ
كَانَ عَاقِبَةُ الْمُجْرِمِيْنَ ﴿۸۵﴾ ع

Na (Tulimtuma) Luti alipowaambia kaumu yake: Je, mnafanya ufasiki ambao hajawatangulieni yeyote kwa huo katika walimwengu?
Hakika ninyi mnafika kwa wanaume kwa kuwaingilia badala ya wanawake, bali ninyi ni watu warukao mipaka!
Na hayakuwa majibu wa kaumu yake isipokuwa wakasema: Wafukuzeni katika mji wenu, maana hao ni watu wanaojifanya wametakasika.
Basi Tukamuokoa yeye na watu wa nyumbani mwake isipokuwa mke wake, alikuwa miongoni mwa wakaao nyuma.
Na Tukawanyeshea mvua (ya adhabu). Basi tazama jinsi ulivyokuwa mwisho wa wakosefu (7:81-85)

NUKUU YA HADITHI

Imesimuliwa na Hadhrat Jabir bin`Abdullah kwamba Mtume wa Allah s.a.w. amesema "Kitu ambacho ninakihofia zaidi kwa umati wangu ni matendo ya watu wa Lut"

Hekima ya Kumsujudia Mtu

Na.
Mwandishi wetu

وَرَفَعَ اَبَوَيْهِ عَلَى الْعَرْشِ وَخَرُّوْا لَهٗ
سُجَّدًا ۚ وَقَالَ يٰۤاَبَتِ هٰذَا تَاْوِيْلُ رُءْيَايَ
مِنْ قَبْلُ ۖ قَدْ جَعَلَهَا رَبِّيْ حَقًّا ؕ وَقَدْ
اَحْسَنَ بِيْۤ اِذْ اَخْرَجَنِيْ مِنَ السِّجْنِ
وَجَآءَ بِكُمْ مِّنَ الْبَدْوِ مِنْۢ بَعْدِ اَنْ نَّزَغَ
الشَّيْطٰنُ بَيْنِيْ وَبَيْنَ اِخْوَتِيْ ؕ اِنَّ رَبِّيْ
لَطِيْفٌ لِّمَا يَشَآءُ ؕ اِنَّهٗ هُوَ الْعَلِيْمُ الْحَكِيْمُ ﴿۱۰۰﴾

[Surat Yusuf 101]

Na akawanyanyua wazazi wake na kuwaweka kitini, na wote wakaporomoka kumsujudia (Mwenyezi Mungu). Na akasema: Ewe babaangu, hii ndiyo hakika ya ndoto yangu ya zamani. Bila shaka Mola wangu Ameihakikisha. Na Amenifanyia hisani aliponitoa gerezani na kuwaleteni ninyi kutoka jangwani baada ya Shetani kuchochea baina yangu na ndugu zangu. Hakika Mola wangu ni mpole kwa Amtakaye. Bila shaka Yeye ni Mjuzi, Mwenye hekima.

DESTURI ya Kuwa sujudia watu ilianza kwa Nabii Adam a.s 2:35 na pia aya hii inaonyesha Nabii Yusuph a.s naye amesujudiwa. Ni nini Hekima yake? Ni kweli inapaswa kuwasujudia Watakatifu? Maneno KHARRUU LAHUU SUJJADAN siyo maana yake kuwa wazazi wa Yusuf na nduguze walikwenda sujuda kumsujudia Yusuf. Maana yake ni kwamba walimsujudia Mwenyezi Mungu kwa ajili ya Yusuf, yaani walimshukuru Mungu kwa kumpa Yusuf cheo kikubwa kama kile.

SUJUDA za namna hii zipo sana katika Desturi za Islamu. Jamaa zako au ndugu zako wanapofanikiwa au kupata cheo basi Jamaa zake huanguka kwa Mwenyezi Mungu kumshukuru Allah kwa Ajili yake. Kwa kuwa Rehema aliyojaliwa itawafaa ninyi nyote. Kwa kuwa Mtume s.a.w ni Rehema ya Ulimwengu basi daima tunapaswa sote kuendelea Kumsujudia/ Kumsalia 33:57 ili Daima Rehema alizopewa na Allah ziwe pamoja nasi. Hii ndio Siri ya Kumsujudia Mtu. Ni kumuomba Allah Akujalie Rehema alizopewa Ndugu yako ziwe sehemu ya Maisha yako. Usipofanya hivyo Rehema za Mtu huwa hazipatikani nawe na kutupwa nje ya Rehema zake kama Ibilisi. Rehema za Allah zimeambatana nyingi na Vuongozi na Wazazi. Kudumu kuwaombea basi unaambatanisha Rehema zao kwako.

Imeandaliwa na Musa Salum 0717504690

Mola wetu, Unighofirie mimi na wazazi wangu na waaminio siku ya kusimama hesabu. Surah 14:42. Amin

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Mwongozo Mkuu, Faida na Fadhila

zisizo na Mwisho za Quran Tukufu kwa Mtazamo wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Kutokaa Uk wa 1..

neza mafundisho hayo duniani. Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba atawasilisha nukuu za Masihi Aliyeahidiwa (as) ambamo anazungumzia umuhimu na adhama wa Qur'ani Tukufu.

Mafundisho Yanayojumuisha Mambo Yote

Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba mafundisho ya Qur'ani Tukufu ni kamili na hakuna ukweli wowote ambao haiufikii. Imeelezwa katika Qur'ani Tukufu:

"Hatukupuuza Kitabuni kitu chochote." (Qur'ani Tukufu, 6:39). Khalifa mtukufu (atba) alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba si kila mtu ana uwezo wa kutoa nukta zote bora na maana zote za Qur'ani Tukufu, bali ni wale ambao ni wapokeaji wa wahyi wa Mwenyezi Mungu na wale ambao wamepewa uwezo maalum na Mwenyezi Mungu ambaye anaweza kufikia maana za ndani kabisa za Qur'ani na kuzitumia kwa nyakati za sasa. Hivyo basi, wale miongoni mwa wateule wa Mwenyezi Mungu ambao juu yao hakika za Qur'ani Tukufu zinaendelea kufunguliwa wanapaswa kuangaliwa ili kupata ufahamu bora na sahihi zaidi wa Qur'ani Tukufu.

Njia Tatu za Mwongozo kwa Wanadamu

Khalifa mtukufu (atba) aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alieleza kwamba Ahadith (maneno ya Mtukufu Mtume (saw) pia hutoa ufahamu na maelezo zaidi ya Qur'ani Tukufu. Mtukufu Mtume (saw) hakuwahi kusema chochote ambacho kilikuwa kinyume na Qur'ani Tukufu. Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Mwenyezi Mungu Mtukufu ametoa mambo matatu kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu; ya kwanza ni Qur'ani Tukufu. Inafundisha daraja tukufu na la juu la Mwenyezi Mungu, na pia inasuluhisha masuala mbalimbali, kama vile yale mabishano kati ya Wayahudi na Wakristo na kufafanua dhana potofu ya Yesu (as) kufa kifo cha laana msalabani. Qur'ani Tukufu inaondoa vipengele vyote vya Shirki (kumshirikisha Mungu). Qur'ani Tukufu inafungua njia za wokovu. Mafanikio yote na wokovu unategemea Qur'ani Tukufu. Hakuna haja ya kiroho ambayo haiwezi kupatikana katika Qur'ani Tukufu. Hakuna kitabu chini ya mbingu isipokuwa Qur'ani Tukufu ambacho kinaweza kutoa njia ya mwongozo. Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Mungu amefanya neema kubwa juu yetu kwa kutumia Qur'ani Tukufu. Lau kuwa Qur'ani Tukufu ingeteremshwa kwa Wakristo, wasingelipotea. Kwa hivyo lazima tushukuru kwa neema hii kubwa na baraka ambayo tumepewa. Ni njia kuu ya kutuokoa. Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba takwimu zinaonyesha kwamba siku hizi, Wakristo wengi zaidi wanaacha Ukristo kwa sababu hawawezi kupata kuridhika kwenye mambo ya kiroho. Inasikitisha kwamba baadhi ya Waislamu wanapuuza Qur'ani Tukufu licha ya kuwa na mwongozo wa mwisho wa kiroho. Khalifa mtukufu (atba) umemnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba ikiwa mtu atafuata amri za Qur'ani Tukufu na kuishi maisha yake ipasavyo, basi Qur'ani Tukufu inaweza kumuwezesha kufuata njia za Mitume. Mwanzoni tu Qur'ani Tukufu inafundisha dua:

"Utuongoze kwenye njia iliyonyooka. Njia ya wale uliowaneemesha'. (Qur'ani Tukufu,1:6 - 7). Wale walioneemeshwa ni manabii, maswiddiq (wakweli), mashahidi na watu wema. Hivyo basi, ni lazima mtu asiiache Qur'ani Tukufu, kwani inatafuta kuwapa baraka zile zile ambazo iliwapa wale waliokuwa kabla yetu. Masihi Aliyeahidiwa (as) alieleza zaidi kwamba njia ya pili ya mwongozo ni Sunnah (matendo ya Mtukufu Mtume (saw) na ya tatu ni Hadith.

Kupata Heshima Kupitia Qur'ani Tukufu

Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba wale wanaoiheshimu Qur'ani wataheshimiwa mbinguni. Qur'ani Tukufu isiachwe kama kitu kilichosahaulika kwani mafanikio yetu ya mwisho yamo ndani yake. Hakuna kitabu kwenye uso wa dunia kwa ajili ya wanadamu isipokuwa Qur'ani Tukufu. Hivyo basi, mtu anapaswa kushikamana nayo ili Siku ya Kiyama ahesabiwe miongoni mwa waliopata wokovu. Qur'ani Tukufu inamwezesha mtu kupambana na ukatili wowote. Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba mfano huu ulionyeshwa hivi majuzi na ndugu zetu waliouawa kishahidi huko Burkina Faso. Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Mtukufu Mtume (saw) alikuwa Muhuri wa Manabii, na Qur'ani Tukufu ni Muhuri wa Vitabu Vyote. Mungu bado anazungumza na milango ya wahyi bado iko wazi, na huu wenyewe ni uthibitisho mkubwa wa ukweli wa Qur'ani Tukufu na Mtukufu Mtume (saw). Inashangaza kwamba baadhi ya Waislamu wanadhani kwamba licha ya kufundishwa swala (dua) ya kukanyaga njia ya wale waliopewa baraka, lakini wanaamini kwamba hakuna yeyote katika Umma wa Kiislamu ambaye kwa hakika anaweza kufikia daraja la watu hao. Hata hivyo, kwa nini Mungu afundishe dua hii ikiwa haikuwezekana kufikia cheo hicho? Kwa hakika inaweza kupatikana, na hili ndilo lengo hasa la Uislamu na Qur'ani. Inashangaza kwamba madai ya kukufuru Qur'ani Tukufu yanatolewa dhidi ya Waahmadiyya, lakini haya ni maoni ya Waislamu wengine kuhusu Qur'ani Tukufu. Ni Waislamu wa Ahmadiyya wanaoshikilia sana imani kwamba Mungu yu hai na bado anazungumza leo kama alivyofanya hapo awali na huu ndio ujumbe unaotaka kuueneza. Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba inaleta maana tu kwamba Muhuri wa Manabii alifunuliwa Muhuri wa Vitabu Vyote; kitabu ambacho kina muongozo wa mwisho, ambacho hakina na hakiwezi kuigwa katika kitabu kingine chochote au maandiko. Ukuu na makamo ya wateule wa Mungu pia vinaonyeshwa katika kitabu kilichofunuliwa kwao. Hakuna anayelingana na Mtukufu Mtume (saw) na cheo chake cha juu, makamo na sifa zake na hivyo ndivyo hali ya Qur'ani Tukufu. Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba wakati hali iko hivi, hakuna mtu ambaye anaweza kuweka madai dhidi ya Ahmadiya akisema kwamba wanavunjia heshima daraja la Mtukufu Mtume (saw).

Andiko Lisilo na Mfano Katika Mafundisho yake

Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba hakuna kitu kinachoweza kulinganishwa na Qur'ani Tukufu, iwe kwa ufasaha, mafundisho, maana, madhumuni, bishara au katika sura nyingine yoyote. Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu zaidi Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Qur'ani Tukufu si mkusanyiko tu wa hadithi. Kwa hakika, hata hadithi ambazo zimetajwa ndani ya Qur'ani Tukufu zinaleta falsafa ya ndani kabisa. Ujuzi wa kina wa Qur'ani Tukufu umewatia msukumo wengi katika upataji wao wa elimu katika sayansi na utafiti wa kisasa. Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba aliona hata ukengeukaji mdogo kutoka kwenye Qur'ani Tukufu na Mtukufu Mtume (saw) kuwa ni sawa na ukafiri. Zaidi ya hayo, Masihi Aliyeahidiwa (as) alieleza kwamba Qur'ani Tukufu ni pana katika upeo wa mafundisho yake. Inafundisha kwamba wakati mwingine, kulingana na hali, ni bora kusamehe, na katika hali nyingine ni busara zaidi kuadhibu ili kurekebisha. Hakuna tofauti kati ya maneno na matendo ya Mungu - Yeye ni Msamehevu, ilhali Yeye pia huwaadabisha waovu pale inapobidi. Jambo hili hili limeakisiwa katika Neno Lake, Qur'ani Tukufu. Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu zaidi Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Qur'ani Tukufu inawasilisha sifa za Mungu kwa namna ambayo inaweza kutambulika duniani. Kurani Tukufu humwezesha mtu kumpata Mungu. Khalifa mtukufu (atba) amemnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba ingawa mafundisho ya Mitume wengine hayawezi kupatikana tena duniani leo, nuru na mafundisho ya Mtukufu Mtume (saw) bado yangali hai duniani leo, kumfanya kuwa nabii wa kweli aliye hai. Nuru ya mafundisho yake iko ulimwenguni leo kama ilivyokuwa hapo awali. Qur'ani Tukufu inawasilisha mafundisho yenye uwiano zaidi, mafundisho ambayo yanawiana na asili yenyewe ya mwanadamu. Kwa hivyo, ni mafundisho ambayo hayalinganishwi na mengine yoyote. Torati inasisitiza kulipiza kisasi, ilhali Injili zinafundisha upole kupita kiasi. Hata hivyo, Qur'ani Tukufu inawasilisha mafundisho yenye uwiano, kwa kusema:

Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao; lakini anayesamehe kwa nia ya kusuluhisha, basi ujira wake ni juu ya Allah … (Qur'ani Tukufu, 42:41) Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) alikuwa akithibitisha ubora wa Qur'ani Tukufu kwa wakati na mahali palipokuwa chini ya utawala wa Kikristo. Kwa hakika hili ndilo lilikuwa lengo hasa ambalo kwa ajili yake Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumwa yaani - kueneza ukweli na kuonyesha ubora wa mwisho wa Qur'ani Tukufu.

Umoja wa Mwenyezi Mungu Uliowasilishwa na Qur'ani Tukufu

Khalifa mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) akisema kwamba kuna baadhi wanaodai kwamba Qur'ani Tukufu haijaleta jambo lolote jipya na inawasilisha umoja wa Mungu kama vile Taurati ilivyofanya. Hata hivyo hii si kweli, kwa sababu Qur'ani Tukufu inawasilisha umoja wa Mungu kwa maelezo mazuri sana na kwa uwazi ambao haujatajwa popote pale kwenye Taurati. Qur'ani Tukufu inaweka ufahamu wa kweli wa umoja wa Mwenyezi Mungu, inaondoa vipengele vyote vya kumshirikisha Mwenyezi Mungu, na inafundisha kuweka upendo wa Mungu juu ya kitu chochote kile. Khalifa mtukufu (atba) alisema kwamba kuna marejeo mengine mbalimbali na nukuu juu ya mada hii ambayo yatawasilishwa katika siku zijazo.

Ahmadiyya Yakutana na Rais wa Zanzibar Dr. Hussein Ally Mwinyi

Kutoka Uk wa 1..

nayo kuelekea kwenye Mkutano huu, Ujumbe huo ulijumuisha Manaibu Amiri wote wawili ambao ni Maulana Sheikh Abid Mahmood Bhutt & Maulana Sheikh Abdur Rahman Ame, Bwana Seif Hassan Nakuchima katibu Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya Tanzania, *Bwana Yahaya Yusuf Kambaulaya, katibu wa mambo ya ndani wa Jamaat Tanzania* na wajumbe wawili wa Mkoa wa Kijamat Zanzibar akiwemo Bwana Said Othman Rais wa Migombani Bwana Mzee Mohammed Mzee Rais wa Tawi la Unguja Ukuu.

Ujumbe wa Jamaat ulifika mapema maeneo ya ikulu kwani muda uliopangwa ulikuwa ni saa nne kamili za asubuhi, hivyo muda ulipokaribia ujumbe uliingia sehemu ya mkutano na Mheshimiwa Rais, lakini waandazi waliandaa sehemu kubwa ya Ukumbi kwani taarifa iliyowafikia ni kwamba ni mkutano na Mashekh hivyo walitarajia jopo kubwa la Masheikh, lakini kwa sababu muda ulikuwepo bado waliamua kundaa sehemu nyingine ambayo ilikuwa nzuri na inayoweza kuwatosha wageni waliofika, ambayo pia ni miongoni mwa kumbi za mikutano za Ikulu. Mnamo saa nne na nusu ndipo kikao rasmi kilianza kati ya Ujumbe wa Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya Tanzania na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe.Dk.Hussein Ally Mwinyi. Ndipo Amiri na Mbashiri Mkuu alichukua nafasi hiyo kutambulisha ujumbe alioambatana nao mbele ya Mhe. Rais, kisha utambulisho wa Jamaat, imani yake, shughuli zake za kiroho na kijamii pamoja na mchango wake katika nchi ulifanywa na Maulana Abdur Rahman Ame Sahib, japo kuwa katika hili kulikuwa na hofu kidogo sawa na uzoefu uliopita kwani watu wa Zanzibar ni wageni kabisa kuhusu Jumuiya na pindi wanapofikishiwa utambulisho kuhusu Jamaat na itikadi zao hushindwa kujizuia na kuanza kujibu moja kwa moja na kubadili sura ya mkutano wa kawaida kuwa mjadala na hiyo ilishawahi tokea mara kadhaa, hivyo basi Amiri na Mbashiri Mkuu alitoa muongozo wa namna Fulani ili kuepusha rapsha za namna hiyo zisitokee tena. Uzuri ni kwamba Mhe. Mwinyi aliweza kubaki katika mlengo wake wa kisiasa na alikuwa muelewa na ustahmilivu kama kiongozi, na hii huenda ni kwa sababu sio Mgeni na Jumuiya sawa na Uzeofu wake alishakutana na Jopo la Jumuiya kipindi akitumikia kama Waziri wa Afya wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Na Mhe. Rais katika maelezo yake alieleza wazi kuwa anatambua mchango wa Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya Tanzania katika mipango yake ya kuisaidia jamii, alisema:

"Na Mimi natambua juhudi zenu na kazi mnazozifanya, sehemu nyingi tunapita tunaona maandishi yanayoonyesha kwamba kisima hichi kimechimbwa na taasisi ya Ahmadiyya, watu wanapata huduma katika jamii zile na suala zima la Afya na Elimu ni maeneo muhimu sana ambayo tunachukua fursa hii kama Serekali kushukuru kwa msaada mnaoutoa kwa Serekali na kuwafikishia wananchi huduma hizi".

Naye Amiri na Mbashiri Mkuu alitoa neno la shukurani mbele ya Mhe. Rais na pia aliongezea kuwa mafundisho yetu ni ya amani na tupo kinyume na hatuungi mkono yeyote ambaye anajaribu kuvuruga amani ya nchi kwa kutumia mafundisho ya Kiislamu.

Baada ya hapo Mhe. Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi alikabidhiwa zawadi ya vitabu kadhaa ikiwepo Qurani tukufu yenye tafsiri ya Kiswahili, kuhusu Qurani hii alielezwa katika utambulisho kuwa Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya ndio taasisi ya kwanza ya Kiislamu ambayo ilifasiri Qurani tukufu katika lugha ya Kiswahili, naye alitoa maoni yake kwamba 'hii ni legacy kwa ajili yenu' akimaanisha kwamba Qurani tukufu ya Kiswahili ni urithi au nembo kwa ajili ya Jamaat Ahmadiyya Tanzania. Pia alipatiwa Hekima ya Mafundisho ya kiislamu, Mgogoro wa Dunia na njia ya kuelekea kwenye Amani na Majibu ya Uislamu kwa Masuala ya Kisasa cha Hadhrat khalifat ul Masihi IV (rh).

Baada ya kikao hicho kilichofanyika kwa hakika katika sura ya kirafiki kabisa huku jopo la Jumuiya ya Waislamu Wahmadiyya Tanzania wakipewa hadhi na stahiki zao zote za ugeni, picha ya pamoja kwa ajili ya kumbu kumbu zilipigwa huku Mhe. Rais akiwasindikiza wageni mpaka nje ya ukumbi na kuwaaga.

Kikao hiki kilikuwa na muitikio mkubwa sana na matokeo mazuri kwani baada ya pale hata wale wasaidizi wa Mhe. Rais walionyesha shauku ya kujua zaidi kuhusu Jumuiya na kuomba nao wapatiwe vitabu hasa Qurani tukufu na vitabu vingine ambavyo vingewatambulisha zaidi kuhusu Jumuiya, baada ya ombi hilo kufikishwa kwa Amiri na Mbashiri Mkuu aliidhinisha papo hapo kwamba wapewe hizo Qurani walizohitaji, na vitabu vingine vilivyohitajika ndungu wa Zanzibar waliamua kuvigharamia wenyewe.

Amiri na Mbashiri Mkuu katika maoni yake alidhihirisha kuwa mkutano huu ulikuwa na matokeo chanya zaidi kuliko mikutano mingi iliyopita kwani vyomba mbali mbali vya habari vilichapisha habari hii. Kwenye gazeti la Zanzibar Leo, picha ya kwenye ukurasa wa mbele ilikuwa kuhusu mkutano huu kwa kichwa cha habari "Dk Mwinyi: tunaunga mkono juhudi za taasisi binafsi", vivyo hivyo kwenye Zanzibar Mail, Mwananchi na pia habari zilirushwa kwenye runinga kadhaa kama ZBC, TBC, ITV nk, pia zilisahishwa kwenye wavuti ya Ikulu Zanzibar na Ukurasa wa Instagram wa Ikulu Zanzibar walisalisha video ya dakika mbili. Hakika mkutano huu umefungua ukurasa mpya wa utambulisho wa Jamaat Ahmadiyya Tanzania na pia umeamsha hari za wanajumuiya kwa namna Fulani. Alhamdulillah.

Mwongozo: Shikeni Hulka Bora

Tafsiri: Sheikh Shahab Ahmad, Morogoro

Hazrat Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema:

"Hulka bora ni muujiza mkubwa sana ambayo inaweza kuwa na umuhimu mwingi zaidi kuliko hata miujiza mingine ya kushangaza akili. Kwa mfano, ikiwa muujiza wa kupasuka kwa mwezi utatokea leo basi mara moja mabingwa wa fizikia na sayansi asili na wapenzi wa sayansi watapenda kupunguza hadhi yake kwa kuujumuisha katika aina za kupatwa kwa jua na mwezi. Na ule muujiza wa siku nyingi unaosimuliwa sasa basi husema kama ni hadithi tu. Kwa mfano, ishara hii ya kupatwa kwa jua na mwezi iliyodhihirika katika Ramadhani na ambayo ilikuwa ishara ya kimbingu kati ya ishara za Imam Mahdi. Mimi nimesikia kuwa baadhi ya watu husema kwamba hii ilithibitisha kwa mujibu wa elimu ya falaki kwamba ishara hii itatokea katika Ramadhani. Kwa kusema hivi wanapenda kupunguza hadhi ya hadithi iliyosimuliwa na Imam Bakir (a.s). Lakini hawa wajinga hawaelewi hata kidogo kwamba kila mtu hawezi kufanya unabii. Unabii ni kufanya utabiri, yaani si kazi ya kila mtu kufanya utabiri. Mtume Mtukufu (saw) alisema kwamba katika zama za Mahdi na Masihi ishara hii ya kupatwa kwa jua na mwezi itadhihirika na hii hadi leo haijawahi kutokea tangu dunia ianze. Hivyo kiakili kama kuna wasiwasi wa aina yoyote basi wapinzani kama hawa wanaombwa kupunguza hadhi ya utabiri huu kihistoria; yaani watoe taarifa ya zama ambapo ilitokea hivi ishara ya kupatwa kwa jua na mwezi katika Ramadhani na pia mtu yeyote alitangaza madai yake kabla. Yaani (watoe taarifa kwamba) mtu huyu alitangaza madai yake na pia utabiri ulitolewa wa kupatwa kwa jua na mwezi katika zama za Nabii yeyote aliyepita; lakini haiwezekani kwa mtu yeyote kutoa taarifa hii.

Lengo langu la kueleza tukio hili ni kwamba kuhusiana na miujiza ya kushangaza akili watu hueleza sababu za aina mbalimbali na hupenda kuidharau; lakini hulka nzuri ni muujiza ambao hakuna anayeweza kuukanusha. Ndiyo maana muujiza mkubwa na mzito kuliko yote uliopewa kwa Mtume wetu mtukufu (saw) ni wa hulka bora."

(Malfuzat, Juz. 1, kur. 140-141)

Jomo Kenyata Na Waahmadiyya-Kenya

Na.
Mahmood Hamsin Mubiru
Kiwalani Dar es Salaam

Katika nchi zote za Afrika ambapo kulikuwa na walowezi wa Kizungu, uhuru katika nchi hizo ulipatikana kwa mbinde (vuta nikuvute) kubwa na utumiaji wa mtutu wa Bunduki. Inzi hufia kwenye Donda wanasema Waswahili ni halali Walowezi hao waliokumbwa na umasikini na kutokana na ushawishi wa Cecil Rhodesia yule bepari aliyeanzisha himaya ya Waingereza huko kusini mwa Afrika waliweza kuichukua Rhodesia ya Kusini (Zimbabwe ya leo), Nyasa-land (Malawi ya leo) na Rhodesia yaKaskazini (Zambia ya leo) na hawakuwa tayari kutoka katika ardhi hizo. Walowezi wengine walipatikana huko Algeria, Msumbiji, Angola na' Kenya. Nzi yuko tayari kufia kwenye kidonda.

Huko Afrika ya kati, Roy Wolensky alifanya jitihada kubwa ya kuunda shirikisho la Afrika ya kati ikiwemo Nyasa land, Southern Rhodesia na Northern Rhodesia ili kunyonya nchi hizo. Hata hivyo jitihada hizo za kupanua wigo wa unyonyaji ziligonga mwamba. Wakina Dr. Hastings Kamuzu Banda, Kanyama Chiume, Chipembere waliungana chini ya Malawi Congress Party ili kupinga shirikisho hilo. Kenneth David Kaunda alipeperusha bendera ya UNIP (United Nation Independent Party) na kupinga shirikisho. Nao akina Joshua Nkomo, Ndabaningi Sithole na Robert Gabriel Mugabe hawakukubali katu njama za walowezi.

Nchini Zimbabwe harakati ziliendelea, Smith akajitangazia uhuru na nchi huru za Kiafrika zikasimama kupinga uhuru huo bandia. Vitimbwi vya Uingereza vilipozidi ikaonekana kuwa ni mtutu wa bunduki tu ambao ungeweza kuleta ukombozi. Vyama vya **ZAA** na **ZANU** viliungana na kuunda Patriotic Front tayari kwa mapambano na walowezi. Hakuna nchi ambayo iliwahi kupewa.

Kama walivyófanya katika nchi za hapo juu, katika Kenya hali kadhalika kama tulivyokwisha ona Uhuru kwenye safari ya Dhahabu walipora ardhi yote nzuri na kuimiliki wao. Lakini haikuwa rahisi kiasi hicho, mapambano yalijitokeza, wenye nchi wakikataa kutawaliwa. Kwa sababu ya silaha dhaifu walowezi wakaikalia Kenya kwa mabavu huku Wakenya wakilazimishwa kufanya kazi katika mashamba ya Walowezi kwa mshahara tonge, kunyanyaswa, kupiga vita mila na desturi za wananchi na kuanzisha shule ambazo kazi kubwa ilikuwa kutukuza Umagharibi kudhalilisha Waafrika. Kadhia hiyo waliyopambana nayo wananchi wa, Kenya imeelezwa na Muandishi maarufu Ngugi wa Thingo katika "Weep not child, The River Between, A grain of wheat, Petals of blood, The Black Hermit-1968, Secret Lives-1976, The Trial of Dedan Kimathi-1976, I Will Marry When I Want-1977, Devil on the Cross -1982, Decolonising the Mind-1986, Moving the Centre-1993, Wizard of the Crow-2006.

Jomo Kenyata katika hali hiyo ya kuzingirwa aliona njia pekee ya kutayarisha jeshi pekee la ukombozi ni kuwa na shule zinazoenzi heshima, utamaduni, mila na desturi za Mwafrika. Yeye aliamini kwamba ukombozi wa kweli wa binadamu unaanza na akili na mtizamo wake. Prison Diary na This Time Tomorrow.

Kama hujajikomboa kichwani, ukombozi wowote mwingine unakuwa hauna maana Shule hizo alizoanzisha Jomo Kenyata zilijitahidi sana kuonesha upotofu wa shule zile za Serikali na za Wamissionari Ni Jomo Kenyata aliyekuwa mstari wa mbele katika



kuanzisha shule hizo zilizojulikana kama Independeney Schools. Na la kufurahisha zaidi ni kwamba shule hizo zilijengwa kwa njia ya kujitegemea bila kutegemea msaada kutoka nje. Shule hizi zilijengwa kwa ule mwito wa 'harambee.

Sheikh Mubarak Ahmad alivutiwa sana na sera hii ya kutaka kujiletea maendeleo na hivyo alizitembelea shule hizo. Yeye aliamini ya kwamba ni jambo la msingi kuwaendea vijana hususani mashuleni akielewa kuwa fikra zao bado ni nyeupe na hazijachafuliwa. Itakumbukwa ya kwamba hivyo ndivyo alivyofanya huko Tanganyika alipokwenda shule ya Tabora ambako aliwaathiri viongozi wengi wa baadae wa nchi hiyo.

Akiwa Kenya Sheikh Mubarak Ahmad alijuana na Jomo Kenyata na akawa anaenda kufundisha dini ya Kiislam katika shule hizo. Ni wakati huo alipopata fursa nzuri ya kuzungumza na Jomo Kenyata juu ya hali ya baadae ya Kenya. Na historia inaonesha ya kwamba baadae walifanya mikutano mingi nchini Kenya kueleza jinsi gani Waafrika wanavyoweza kupata ustawi.

Mikutano ya mara kwa mara baina ya Jomo Kenyata na Sheikh Mubarak Ahmad ilijenga urafiki mkubwa na wa kuheshimiana. Kenyata alielezwa juu ya maisha matakatifu ya Mtukufu Mtume Muhammadsaw na jinsi alivyowatetea wote waliokuwa wanaonewa kwa pamoja walikubaliana juu ya mikakati ya wananchi wa Kenya kudai haki zao. Sheikh Mubarak Ahmad aliamini katika sera ya kuwaambia wakoloni' uonevu waliokuwa wanafanya kwa kuwanyang'anya ardhi, kuwabagua, malipo madogo, mbinu zilizokuwa zinatumika ili watu walipe kodi, utembeaji na kipande. Mbinu zilizokuwa zinatumika katika kulipa kodi, utembeaji na kipande kikionesha ya kwamba una kazi au la sivyo urudi kijijini. Hayo yote Sheikh Mubarak Ahmad aliona ni maonevu na ndio maana aliunga mkono harakati za uhuru wa **Kenya**. Hata hivyo "akiwa kiongozi wa Kidini aliwaambia wananchi wanaodai uhuru wautafute kwa amani na kwa kuzingatia sheria. Historia ya baadae inaonesha ya kuwa Jomo Kenyata ingawaje alifungwa kwa madai ya kuanzisha, kuendeleza mapigano ya msituni Maumau, hata hivyo Mahakama ilimkuta hana hatia. Katika masingizio hayo hakuwa peke yake, bali alifungwa na Bilda Kagia, Achieng Oneko, Paul Ngei, Kungu Karumba na Fred Kubai. Akiwa korokoroni Jomo Kenyata, Sheikh Mubarak Ahmad aliomba ruhusa ya kuonana naye. Ikumbukwe ya kuwa ilihitaji ujasiri wa hali ya juu kujinasibisha kwa njia moja au nyingine na mfungwa wa kisiasa/Serikali ya Kikoloni ilimuona ni mtu hatari na anayehatarisha amani ya Kenya. Sheikh Mubarak Ahmad alikuwa akienda mara kwa mara akimpatia magazeti ya Mapenzi ya Mungu na East African times. Tafsiri ya Qur'an Tukufu ya Kiswahili ilipotoka mwaka 1953 Kenyata alipelekewa nakala amabayo amesema yeye mwenyewe kuwa ameisoma yote zaidi ya mara mbili. Na ilimuathiri sana. Na historia ya baadae inaonesha ya kwamba alitoa ahadi humo humo jela ya kutokunywa Pombe na kula Nguruwe na yote haya aliyatimiza baadae. Jomo Kenyata ni Kiongozi pekee wa Afrika Mashariki ambaye jina lake limo katika sehemu ile ya maelezo ya Qur'an Tukufu uk..... (juu apomhe) Unaeleza juu ya madhara ya Pombe.

Wakati akienda kumtembelea gerezani, walizungumza mengi na alimueleza ya kwamba kwa nguvu za Mwenyezi' Mungu naye akifanya maombi anaweza kuachiliwa huru. Upo ushahidi ya kwamba alikuwa ameanza kusali sala ya Kiislam. Hata hivyoo ilikuwa ni kazi ngumu kuamini utabiri huo kwa kuwa wakati huo kulikuwa na machafuko makubwa na umwagaji wa damu. Sheikh Mubarak Ahmad aliendelea kumfariji kani alikuwa akiamini kuwa alikuwa akitetea haki za wananchi wenzake wa Kenya.

Jumuiyya ya Ahmadiyya katika Kenya ilichukua njia ya uadilifu mkubwa. Haikusita kuiambia serikali mahali ilipokuwa ikiwanyanyasa Waafrika. Ujasiri huo ulitokana na mafundisho ya ya Islam kuwa; 'Kusema haki mbele ya Mfalme ni Jihadi kubwa'. Waafrika nao waliambiwa kuwa walikuwa na haki ya kutetea haki yao lakini sio kwa fujo na vurugu kwani hayo sio mafundisho ya Islam. Kila njia ya halali iliyotumiwa na Wananchi iliungwa mkono na Jamaat. kwa mfano viongozi wa Kenya African Union (KAU) Chama kilichokuwa kinaongozwa na Jomo Kenyata walipotoa tamko lao la kudai haki, gazeti la Kiingereza lililokuwa linatolewa na Jumuiyya ya Ahmadiyya "East African Times' lilichapisha tamko hilo. Hatua hiyo ilikasirisha serikali ya kikoloni na gazeti likafikishwa Mahakamani. Mhariri wa gazeti hilo alitakiwa aombe radhi lakini alikataa. Kwa hiyo gazeti lilitozwa faini na ikalipwa.

Siku Kenyata alipoachiliwa huru ilikuwa ni siku ya kumshukuru Allah na kufurahi. Sheikh Mubarak Ahmad akiongozana na Waahmadiyya alikuwa miongoni mwa wananchi wa Kenya waliokwenda kumkaribisha nyumbani kwake Gatundu. Umati ulikuwa mkubwa. Watu wakiimba na kusherehekea. Katika wingi huo wa watu Jomo Kenyata alimuona Sheikh Mubarak Ahmad akamuita wakakumbatiana na akamuomba aseme maneno machache kwa umati ule. Sheikh Mubarak Ahmad alisema; "Shukrani zote ni za Allah, Aliyemtoa Kiongozi wetu mpendwa gerezani. Tuendelee kumuombea na tuzidi kuiombea nchi yetu Kenya ili ipate ustawi na amani. Njia sahihi ya kutoa shukrani ni kuwapenda watu wote na kuwaheshimu.

Hotuba hiyo fupi ilishangiliwa sana na umati wa watu. Mara tu baada ya hotuba Jomo Kenyata alimkaribisha sheikh MubarakAhmad na ujumbe wake akiwemo Sheikh Muhammad Munawwar ndani kwa mapenzi. Na kabla hawajaingia ndani Wananchi walielewa mafundisho ya Ahmadiyya.

Bustani ya Washairi

NIMEHAMU

Nakuita ewe Rabu, Mlezi wa kila zama
Muda watupa adabu, Uchaji moyoni wahama
Hatuiiti adhabu, Ila dira sio njema
Nimezihamu dhahabu, Zenye tulizo la roho

Nimezihamu za kale, Nyakati za ufikisho
Ilipomweka miale, Ya hamu za uamsho
Zilipozimwa kelele, Pinzani mwenye Vitisho
Jamat Ikawa mbele, Kwa hoja na uthibiti

Nimezihamu salatu, Zenye kwikwi na Hushu'u
Na naziondoazo kutu, Sajidaze na rukuu
Yenye kusogeza mtu, Kwa Molaye na nukuu
Salatu chanzo cha utu, Kimatendo Ukikimu

Nimewahamu Vijana, Wenye Jununi ya dini
Kimatendo waungwana, Mwenye hari na fununi
Kwenye kazi waungana, Kuichuma akherani
Nimeihamu safina, Ilo tuvusha Kitonga

Nimewahamu Wazee, Watiao tumaini
Walosema tuhemee, Riziki ipo miguni
Na upuzi tukatae, Dhalimu si wa peponi
Yalo mazuri tuchukue, Hata kwa aliye duni

Nimemhamu bashiri, Mwenye hima juhudi
Mwenye nguvu tele hari, M'bobezi itikadi
Takwa afuka uturi, Alohini ufisadi
Kaongaza msitari, Kutumikia Jamat

Nimezihamu tadhima, Kwa wenzetu Watumishi
Ajapo twalisimama, Kumlaki kwa matashi
Kauli yao hatima, Hatubadili tamshi
Tukazichuma neema, Zinazotufaa leo

Nimezihamu habari, Zenye mapenzi na huba
Bwana Fulani mahiri, Mkarimu mwenye hiba
Fulani katoa dinari, Amelipwa kwa vibaba
Kajitahidi bukhari,Kujinasua kuchani

Jama lile tabasamu, Lililo Nuru halisi
Liualo uhasimu, Lenye kufuta nuksi
lifikishalo elimu, Yenye sadaka fanisi
Libashirio fahamu, Zenye busara nyingi

Nimezihamu nguvu, Ushauri na hamasa
Mtu akupe makavu, Bila ndimi kupepesa
Akupe kwa utulivu, Majeraha kutogusa
Ushauri angavu, Nyoofu na wenye tija

Nimezihamu amsha, Kuleta mafanikio
Wepesi kiti kalisha, Waharakishe mgao
Gao mapema fikisha, Kwa uzuri so tishio
Chapu mambo kamilisha, Yapo mengine mbeleni

Nimezihamu Jamaa, Zenye uamsho ndani
Khudamu Ijtimaa, Ilo ghera rohoni
Jalsani twajamaa, Twajitoa duniani
Kuhudhuri twapania, Udhuru ni fikira tu

Shunda Mshundia Wana
Daluni - Tanga

Mke uwe Kobe

Mke uwe Kobe, papara ondoye
Sifanye ubabe, japo nguvu jaye
Nyumbayo ibebe, aibu sitiye
Mke uwe Kobe, ndoa ipendeze.

Maneno sijaye, uweke nukita
Sauti sipaye, kavuka ukuta
Neno fikiriye, kabula kutoka
Mke uwe Kobe, ndoa ipendeze.

Nje ukitoka, sitara ivaye
Chini kudondoka, jicho lyangaliye
Mwendo waharaka, mapema rejeye
Mke uwe Kobe, ndoa ipendeze.

Na.
Masihi omary stambuli kisagwa

Bismillahr Rahmaanir Rahiim
Mashaidi wa Afrika

Wamekua mashahidi, wana wa 'Zinjibani'
Kenda yao ni idadi, walioifia dini
Wafuasi wa Mahadi, Afrika Machweoni
Uwapokee Rabuka, Mashahidi wa Afrika

Wafuasi wake nabi, wameiakisi shani
Ni wana wa Bokinabi, walowekwa kafarani
Wamekihami Kitabi, wakajikuta kifoni
Uwapokee Rabuka, Mashahidi wa Afrika

Wana walio stadi, hilo halina ubishi
Wakakabili Jihadi, bila hata panikishi
Kutomkana Mahadi, hilo ndilo lao tashi
Uwapokee Rabuka, Mashahidi wa Afrika

Lengo wakalithabiti, mbele yao magaidi
'Wakapigwa' nyingi 'biti', kamwe hawakuritadi
Tena wakajizatiti, kumhami Ahmadi(as)
Uwapokee Rabuka, Mashahidi wa Afrika

Wote kenda 'nasrini', walofuzu kwenye dini
Wasaidizi makini, njia Yake Rahmani
Walotekeleza dini, kwa hushui na Imani
Uwapokee Rabuka, Mashahidi wa Afrika

Iburahim Bidiga, Imara alisimama
Kamwe hakulegalega, kumwelezea Imama
Hakuwapea kibega, kwa hoja aliwazima
Uwapokee Rabuka, Mashahidi wa Afrika

Na timu yako Bidiga, kamwe haikukwangusha
Walisimama kibega, kufikisha mnakasha
Suhufa wakazimwaga, pasi hofu ya Maisha
Uwapokee Rabuka, Mashahidi wa Afrika

Machozi yatudondoka, damu yenu kumwagika
Myoyo yatutononeka, dunia mmetoweka
Kwa Mola Mwenye fanaka, vifo vyenu vyatajika
Enyi nyota wa Afrika, vifo vyenu vyatukuka

Ya Rabbi Mola Azizi, Muhifadhi Mwenye enzi
Twakwomba bila ajizi, mashujaa Uwaenzi
Utujalie na sisi, tuwe na hatima hizi
Uwapokee Rabuka, Mashahidi wa Afrika

Katu Hawi Mshindani

Kushindwa na kuheshimu, alama ya kujaribu
Tena wapata elimu, yakutafuta majibu
Kunachungu kuna tamu, Ndivyo kapanga wahabu
Asiyependa kushindwa, Katu sio mshindani.

Kushindwa kuna utamu, Niutamu wa ajabu
Kwani unapata hamu, yakuzijua sababu
Zilizo fanya magumu, Ukashindwa yaratibu
Asiyependa kushindwa, Katu sio mshindani

Kushindwa hasa muhimu, tena unamatibabu
Unapata ufahamu, njia ilo twaibu
Silatwa musitakina, iso shaka wala tabu
Asiyependa kushindwa, katu sio mshindani

Mahmood Hamsini Mubiru **(WAMAMBA)**
Kiwalani Mgombani.

SIRI YA CHAKULA

1. Chakula ni mlo, ule uridhike
Kidogo ukile, tumbo sivimbike
Ushinde ulale, uvivu kushike
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe.

2. Ule cha nafuu, lishe kilojaa
Dona si pilau, mboga na dagaa
Chai karafuu, soda takuua
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe.

3. kula kuhusudu, ndugu takukimbia
Uchoyo si budi, kando utupia
Ulafi kizidi, maradhi ugua
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe

4. kula kikuzidi, kipato chujuka
Mwenyewe jifisidi, kula ukishika
Wafanya fisadi, njaa tokutoka
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe

5. Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe
Ukipata faradhi, kipato kikata
Mungu mkabidhi, akiba kukata
Kwa mlo baadhi, jamaa kupata

6. leo si pumbaze, kesho ipuuza
Sinia ujaze, machipsi kwa pweza
Njaa si iweze, kesho takuliza
Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe

7. Mlo ni faradhi, Kiasi kiliwe
Uko njaa ule, ukishiba acha
Kimoja usile, vya gharama acha
Wasitani ule , kuzidisha acha

Masihi Omary Kisagwa

Asherati Hawara Fasiki

Na.
Mwandishi Wetu

UASHERATI ni Uzinifu usio kuwa na Mtu mmoja wa Kuzini naye. HAWARA ni Uzinifu wa Kujenga Kibanda yaani kuwa na Mtu mmoja.

UFASIKI kwenye aya hii 4:26 ni UASI na ASIYEHIFADHI vitu vyake vya MMEWE. Mwanamke MGWANA HAPASWI KUVUNJA UTII na Akivunja Aonywe 4:35

Wanaume ni walinzi wa wanawake kwa sababu Mwenyezi Mungu amewafadhili baadhi yao kuliko wengine, na kwa sababu ya mali zao wanazozitoa; basi wanawake wema ni wale wenye kutii, wanaohifadhi (hata) wasipokuwapo (waume zao) yale Aliyohifadhi Mwenyezi Mungu. Na (wanawake) ambao mnaogopa uasi wao, basi waonyeni na waacheni peke yao katika vitanda, na wapigeni. Na kama wanawatii, basi msiwatafutie njia. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Aliye juu, Mkuu. MNAO MILIKI MIKONO YENU YA KIUME Ni watu wote unaokaa nao nyumbani kwako wasio sehemu ya Familia yako. Kiujumla yeyote anayeingia kwenye Familia ya Mtu anapaswa kuwa chini ya Mkuu wa Familia na ndivyo hata Sala mwenye Mamlaka ya Kuongoza Sala anapokuja Mtu yeyote au mazingira ya nyumbani ni BABA yeye ndiye IMAMU MKUU wa Familia na yeyote anayeingia au kuja kwako anakuwa chini yako. Watu hao unaokaa nao hao Wanaitwa Unawamiliki kwa sababu hiyo. Mjakazi ni Mtumishi wa ndani wa Familia yako, leo ni ma House girl Maana hiyo ilikuwa ya Utumwa ila sasa hakuna Utumwa na Ujakazi umebaki wa House girl vinginevyo aya na maana hiyo haipo tena.

Pia Mtumwa kwa sasa ni Mfanyakazi. MJAKAZI yaani ملكت Linatokana Na Neno ملک Utawala. Ambaye anaweza kuwa Mtumwa au Mtu anayetawaliwa au House girl.

Hii ni Tafsiri ya Neno MJAKAZI lenyewe lilotumika kwenye Quran Tukufu. PIA nimeuliza Wataalamu wetu wameniambia MJAKAZI wa leo ni HOUSE GIRL. Alhamdulillah.

Tafsiri ya MJAKAZI kwa Kiswahili yawezekana ikawa tu MTUMWA ila Ukitaka kujua maana halisi ya Tafsiri tafuta Hilo Neno limetumikaje kwa KIARABU na Jaribu kutafuta maana zake kama zilivyo tumika kwenye Quran Tukufu. Kwa maana hii soma sana Quran Dictionary Tuitafsiri Quran Tukufu kwa Kiarabu chake na sio Neno la Kiswahili lilotafsiriwa ndio Tutake Tafsiri yake. Mzizi hasa huondoka. Na ndio maana Dua za Quran Tukufu inapendeza Kuisoma kwa Lugha zake maana kuna Maana nyingine nyingi zimedichikana ndani yake. Mfasiri hufasiri kwa maana moja aliuokusudia tu Masih Aliyeahidiwa a.s alisema aya moja au Neno moja kwenye Quran Tukufu linaweza fasiriwa kwa maana hata zaidi ya 10 Na bado ikasimama kwa maana yake ile ile Nafikiri kuna Utata wa Lugha mbili ndugu yangu Ukitumia Kiswahili Kufasiri MJAKAZI na Mimi nikitumia KIARABU. Kwa mantiki hii hatuwezi pata Jibu moja.

Ila kwanini Nimetumia Kiarabu Kufasiri MJAKAZI ni kwa sababu Neno lenyewe la ملكت lilofasiriwa kwa maana ya MJAKAZI ni la KIARABU.

Kanuni za Lugha zote maana ya Jambo lolote huwa haipatikani kwa FASIRI yake ila kwa ASILI ya LUGHA yake. Malakat maana yake si mjakazi. Neno la kiarabu kwa ajili ya mjakazi ni عمة Hiyo si maana sahihi, MALAKAT AYMAANAKUM, ni neno la jumla likimaanisha wote unaowamiliki, mjakazi ni miongoni mwao tu. Mjakazi ni mtumwa wa kike Hapana housegirl siyo mjakazi Housegirl anaitwa khaadimah Pia kwa kiarabu mtumishi wa nyumbani anaitwa « Shaghaala» Mjakazi ama Suria ni tafauti kabisa na HOUSE GIRL Kwa maana House Girl ana uhuru wa kuondoka au kuwacha kazi au kuwachishwa kwa wakati wowote sawa na sheria. Mwl Sahib samahani nimetafuta sana aya yenye kutumia Neno hili la عمة kwa maana ya MJAKAZI ila nimepata aya nyingine 24:34 yenye Kutumia MALAKAT kama MJAKAZI.

Naomba aya yenye kutumia neno hili عمة kama MJAKAZI INISAIDIE kwenye Utafiti wangu, Inshaallah Tatizo sio MJAKAZI ila MJAKAZI amebeba sura nzima ya Mjadala wote. Huku tukisahau kuwa SWALI la msingi ni aya ya 4:26 ambapo Neno MJAKAZI limetumika. Mlizaji alipouliza MJAKAZI ni nani ni kamjibu kwa sasa ni House girl Jibu hili ndilo liliozua mjadala. Bila shaka ni Jibu sawa na aya husika na sikujibu sawa na MAANA ya MJAKAZI.

Na bahati mbaya mjadala umeacha Mantiki ya maana ya aya na kujadili maana ya MJAKAZI Nilikosea spelling neno ni امة(ammat) tazama 2:223 Katika aya 24:33 MJAKAZI Ameitwa MTUMWA kwa Neno امة(ammat). Ila aya inayofuatia ya 24:34 MJAKAZI Ameitwa kwa MALAKAT.

Hapa Kuna maana mbili zilizokusudiwa kwa watu hawa Wajakazi.

Na maana ya aya 4:26 hakutumia امة (ammat) bali MALAKAT ambapo MJAKAZI huyu sio LAZIMA AWE MTUMWA Hapana, neno malakat kama nilivyokwiaeleza lina maana pana zaidi, hata binti unayemlea ambaye si nduguyo wa damu anaingia katika malakat Mateka wa kivita pia hingia katika MALAKAT

Na kama mkiogopa kwamba ninyi (kama jamii) mtashindwa kufanya uadilifu katika mambo yahusuyo mayatima baada ya matukio ya vita, basi oeni wanawake wa chaguo lenu wawili au watatu au wanne. Lakini mkiogopa kuwa hamwezi kufanya uadilifu, basi (oeni) mmoja tu, au wale ambao mikono yenu ya kuume imewamiliki; Hii ndiyo njia ya karibu zaidi kwa ajili yenu ili kuepukana na kutokufanya uadilifu. Surah An-Nisaa 4 : 4 Watu hawa walipatikana katika vita zama za Mtume s.a.w. wakiwa ni mateka.

Pia wengine walipatikana baada ya kubaki mayatima.

Waislaam waliishi nao na kuwalea kama sehemu ya familia zao.

Kwa hiyo kama mtu alimtaka yeyote ili awe mke wake aliruhusiwa kufanya hivyo. Siomsichana wakazi, kwa sababu msichana wa kazi ni mtu huru na yupo kwako kama mfanya kazi na unamlipa mshahara.

Lakini hawa wanaosemwa na Quran ni mateka wa vita ambao watu waligawiwa baada ya vita na ili awe huru ni lazima ajikomboe au akombolewe sawa na makubaliano kwa kifupi huyu anakua ni mali yako mpaka atakapo jikomboa.

Sasa huyu ukitaka awe mke wako hakuna pingamizi unaoa tu.

Pia kwa sababu ya vita mayatima walikua wengi sana katika jamii ya Kiislaam hivyo kwa ajili ya ustawi wao walikua wakichukuliwa na Waislaam na kuwajumuisha katika familia hawa pia kama kuna binti na umependa awe mwandani wako hakuna wa kukuziwia kwa sababu ni mali yako. Inaswihi ila huyu mlolongo ni mrefu kidogo sio sawa na hawa wanaozungumzwa katika Quran.

House girl bila shaka atakua na wazazi au ndugu. Tofauti ni hii

Lazima akubali kuolewa nawe.

Lazima mahari

Waliii wake lazima awepo ili atoe idhini

M a s h a h i d i .

Lakini huyu wa kwenye Quran hakuna haja ya Mahari wala walii Unaowa tu.

Jinsi ya Kutengeneza ButterCream ya Kupambia Keki

Mahitaji
-Siagi isiyokuwa na chumvi gram 150
-Icing Sugar Gram 500
-Arki ya vanilla kijiko kimoja cha kulia
-Rangi chakula ya kiasi tu inategemea na wewe mwenyewe unataka ikolee vipi nyingi au kiasi tu au pia unaweza ukatumia rangi nyengine yoyote unayopenda wewe ya chakula
-Maziwa ya maji ya kawaida vijiko viwili mpaka vinne vya kulia
-Sprinkle (vinapatikana Supermarket vimekaa kama vipipi flani)

Maelezo
Chukua Bakuli tia Siagi yako anza kusaga kwa mashine ya cake au mwiko wa kusongea ugali mpaka ibadilike rangi iwe cream.

Baada ya hapo achia kusaga mimina Icing Sugar yako na Endelea kusaga mpaka uhakikishe Icing Sugar imechanganyika vizuri

Baada ya hapo achia kusaga tia arki ya vanilla au yoyote unayopenda wewe mwenyewe pamoja na Rangi ya chakula yoyote unayopenda wewe mwenyewe pamoja na Maziwa ya maji ya kawaida
Endelea kusaga mpaka uhakikishe rangi yako imechanganyika vizuri

Chukua cake yako ikate sehemu ya juu kabisa kama imevimba na kama haijavimba si lazima kuikata.

Anza kuieneza Cake yako ButterCream juu na pembeni halafu iweke sawa kwa kutumia Spatula au Kisu cha kusawazishia Cake iwe smooth vipo special na vinapatikana maduka ya vifaa vya Cake (au unaweza ukaipamba zaidi)

Baada ya hapo ipake sprinkle Jemmy juu (sprinkle hizi zinapatikana supermarket vimekaa kama vipipi flani)

Baada ya hapo unaweza ukaiweka kwenye fridge cake yako ili ipate kukazana isigande ipate baridi tu

Baada ya hapo itoe cake yako kwenye fridge
Na mpaka hapo cake yako ipo tayari kwa kula ni rahisi sana

Adabu za Vikao na Athari zake za Utoro

Na. Mwandishi Wetu

إِنَّمَا الْمُؤْمِنُونَ الَّذِينَ آمَنُوا بِاللَّهِ
وَرَسُولِهِ وَإِذَا كَانُوا مَعَهُ عَلَىٰ أَمْرٍ
جَامِعٍ لَّمْ يَذْهَبُوا حَتَّىٰ يَسْتَأْذِنُوهُ ۚ
إِنَّ الَّذِينَ يَسْتَأْذِنُونَكَ أُولَٰئِكَ
الَّذِينَ يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَرَسُولِهِ ۚ
فَإِذَا اسْتَأْذَنُوكَ لِبَعْضِ شَأْنِهِمْ فَأْذَن
لِّمَن شِئْتَ مِنْهُمْ وَاسْتَغْفِرْ لَهُمُ اللَّهَ ۚ
إِنَّ اللَّهَ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٦٣﴾
لَّا تَجْعَلُوا دُعَاءَ الرَّسُولِ بَيْنَكُمْ
كَدُعَاءِ بَعْضِكُم بَعْضًا ۚ قَدْ يَعْلَمُ اللَّهُ
الَّذِينَ يَتَسَلَّلُونَ مِنكُمْ لِوَاذًا ۚ
فَلْيَحْذَرِ الَّذِينَ يُخَالِفُونَ عَنْ أَمْرِهِ
أَن تُصِيبَهُمْ فِتْنَةٌ أَوْ يُصِيبَهُمْ
عَذَابٌ أَلِيمٌ ﴿٦٤﴾

[Surat An-Nur 63 - 64]

Waaminio ni wale waliomwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake; na wanapokuwa pamoja naye kwa jambo linalohusiana na wote, hawaondoki mpaka wamwombe ruhusa. Kwa yakini wale wanaokuomba ruhusa, hao ndio wanaomwamini Mwenyezi Mungu na Mtume Wake. Na watakapokuomba ruhusa kwa ajili ya baadhi ya kazi zao, basi mruhusu umtakaye miongoni mwao, na uwaombee ghofira kwa Mwenyezi Mungu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Msamehevu, Mrehemevu.
64. Msifanye wito wa Mtume baina yenu kama wito wa ninyi kwa ninyi. Hakika Mwenyezi Mungu Anawajua miongoni mwenu wale waondokao kwa utoro wakijificha. Basi wajihadhari wale wanaokaidi amri Yake, isije ukawapata msiba au ikawafikia adhabu iumizayo.

VIONGOZI Huandaa Vikao kwa Ajili ya Mashauriano kadhaa na Mashauriano ndio KIINI cha Taasisi husika, hivyo Utaratibu huu usingeachwa bila kuwekewa utaratibu. Kwakuwa Vikao ni Muhimu katika Mustakabari wetu basi:

Kwanza Muhudhuriaji / Mjumbe wa Kikao Aombe RUHUSA kwa Mwenyekiti wa Kikao kama Atakuwa na UDHURU na Mwenyekiti Ataweka Utaratibu wa Kuwaruhusu Sawa na Udhuru wao, Akisha mpatia Ruhusa basi Mwenyekiti Atakiwa Kumuombea MAGHOFIRA. Kwanza kwa Mjumbe huyo kukosa Kikao ili mchango wake uweze kuletwa na Mwingine pia Allah Amuondolee Udhaifu huo siku zingine Ahudhurie Asiwe na Udhuru wa kutoa.

Sawa na Haja Mwenyekiti wa Kikao anaweza pia Asitoe RUHUSA ya Udhuru wowote kwa HEKIMA YAKE Husika, Hapo sasa Wafuasi wanatakiwa Kutii ila Nidhamu ya Utii isipozingatiwa HUTOROKA Wasije au Kuondoka kwenye Vikao. Hapo ndipo Allah Anasema MTORO wa Vikao Atapatwa na MSIBA AU ADHABU

Tusijitengenezee Mabalaa ya Misiba na Adhabu kwa Utoro kwenye Vikao na Viongozi Wasiwatengenezee Wafuasi wao Sababu ya Ukafiri za Kuwanyima RUHUSA. Itambulikane ni Kiongozi Anaweza kuwa Rehema kwa watu wake au Akajitahidi Kuwaua Kiimani. Sawa na Kanuni IMANI Hutangulia kwanza ndipo Matendo ya Kiimani Hufuata na ndipo Adhabu hupatikana kwa Mtu Aliyena Imani. Hivyo Viongozi Wawajengee Imani wafuasi wao panapokujiridhisha Wamejengeka Kiimani hapo hawana sababu ya Kujikarifisha kwenye Kanuni.

Tunamuomba Allah Atujalie Kila Mmoja wetu Atuweke kwenye Kutimiza Wajibu wake wa Msingi katika Dini. Amin

Asemavyo Masihi - Sababu ya Kudhalilika ni Kiburi

Hazrat Aqdas Masih Mau›udi anasema: Ninasema kwa ukweli kabisa kwamba siku ya Kiyama, baada ya Shirk hakutakuwa na balaa zaidi ya Kiburi. Hili ni balaa ambalo humdhalilisha Mwanadamu Duniani na Akhera. Rehema ya Mwenyezi Mungu humzunguka kila yule anayeamini umoja wa Mungu isipokuwa mwenye Kiburi. Hata Shetani alikuwa akisema kuwa anaamini umoja wa Mungu, lakini kwa kuwa ndani ya kichwa chake mlikuwa na kiburi, na alipomtazama Adam, Aliyekuwa akipendwa na Mwenyezi Mungu, kwa mtazamo wa dharau na kumkosoa, basi, akaangamizwa na kongwa ya laana ikavikwa shingoni mwake. Hivyo Dhambi ya kwanza iliyomuangamiza mile le Mtu ilikuwa ni Kiburi. (Aina Kamalate Islam, Ruhani Khazaain, J., uk. 598)

Ukichunguza vyema Tunapenda Kuona wenzetu wana Kiburi. Kwa kuwa yale wanayoyafanya yanatukera.

Ila jichunguze mwenyewe Huna chochote unacho Miliki kati ya Heshima yeyote, Maarifa yeyote, Kazi yeyote, Mali yeyote, Afya yeyote, Mke mzuri, Watoto n.k Kisha Ukavitumia kwa njia yeyote yenye maana ya *Kujikweza nacho, Kujifaharisha nacho, Kujitukuza nacho, Kujigamba nacho, Kuringa nacho, Kutopenda Kudhalilishwa nacho, Kutojionyesha MNYONGE kwa kuwa unamiliki moja ya hicho, Kutoishi katika Umasikini kwa sababu tu unamiliki miongoni mwacho?

BASI TUJITAMBUA ama Mimi au wewe tunakiburi. Na Viburi hivi ni Vingi baina yetu na hatari kwa maana ni vipo Karibu na maisha yetu kuliko ya Kiongozi ambapo Kiburi chake mpaka Mkutane kwenye kona yake. Maisha hayo ni machache kuliko maisha yetu ya kila siku.

MATUKIO KATIKA PICHA



Picha ya pamoja ya Raisi wa Zanzibar na wawakilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya siku ya matembezi. Wa kwanza kulia akiwa ni Katibu Umur Ama Yahaya Y. Kambaulaya, wa pili Katibu Mkuu Seif H. Nakuchima, wa tatu Mwl. Said Othman, wa nne Naibu Amir Sh. Abdul-Rahman M. Ame, wa tano wa tano Raisi wa Zanzibar Dr. Hussein Ally Mwinyi, wa sita Amir Sahib Sh. Tahir M. Chaudhry, wa saba na wa saba Naibu Amir Abid M. Bhatti, nane na wa mwisho Mr. Mohammed Mzee Rais wa Tawi la Unguja Ukuu



Mauwaji ya Mashahidi tisa katika picha Mjini Abad – Burkina Faso waliouwawa siku ya Tarehe 11. Januari 2023. Yalitolewa katika Muhtasari wa Hotuba ya Ijumaa ya Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tanoatba iliyotolewa katika Masjid Mubarak, UIngereza. Tarehe 20 Januari, 2023. Mashahidi (wa dini) wa **Burkina Faso – Nyota tisa za Ahmadiyya.**

Kalamu kutoka Kanda ya Ziwa

KUCHANUA KWA CHEMCHEM YA JAMAAT AHMADIYYA MKOANI SHINYANGA - 1



Yousuph Mgaeleka (Muijukuu)

Ilikuwa ni mwanzoni mwa mwaka 2012 pale ambapo kiongozi wetu mpendwa nchini Mheshimiwa Amir na Mbashiri Mkuu nchini Tanzania Maulana Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry alipofanya ziara mkoani Mwanza, lengo likiwa ni kuja kuhudhuria na kushiriki Mkutano wa Amani yaani (Peace Conference) uliokuwa umeandaliwa siku ya jumamosi na wanajumuiya wa mkoa wa Mwanza. Mkutano huo ulipangwa kufanyika katika moja ya Hotel jijini humo ijulikanayo kama (Gold Crest Hotel). Ambapo kiongozi wetu mpendwa Amir Sahib alitenga muda wake na kuamua kusafiri kuja kuhudhuria na kuongoza mkutano huo wa siku moja jijini Mwanza, mkutano ambao ulihudhuriwa pia na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza wa wakati huo ndugu Evarist Ndikilo. Katika mkutano huo ulijumuisha pia wageni waalikwa mbalimbali kuhudhuria wakiongozwa na wanajumuiya wenyeji, ama kwa hakika mkutano ulifana sana Alhamdulillah. Nakumbuka kiongozi wetu Mheshimiwa Amir Sahib alitoa khutba rasmi ikiwa ni ufunguzi wa mkutano huo wa Amani, na kuwasihi washiriki wa mkutano huo kuilinda Amani huku akitoa hamasa kubwa ya kuepusha ukatili wa mauaji ya vikongwe na walemavu wa ngozi yaliyokuwa yameshamiri katika ukanda wa Ziwa. Hakika khutba yake ilivutia sana na hata Mheshimiwa MKuu wa Mkoa wa wakati huo aliwekea mkazo sana aliposimama nae kuhutubia hadhira hiyo. Hafla hiyo ya Mkutano wa Amani iliendelea mpaka majira ya saa mbili hivi usiku ambapo ndio ulifikia kilele chake na hitimisho, na ilishirikisha jumla ya wanajumuiya na wageni waalikwa wapatao 200 hivi. Mkutano huo ulihitimishwa kwa maombi ya kimya kimya yaliyoongozwa na Maulana Amir sahib.

Ndugu zangu wapendwa, kumbe ujio huo wa Amir sahib ilikuwa ni muongozo wa Allah katika kuufungua ukanda wa Ziwa kijamaat. Ilikuwaje sasa…..

Mara baada ya kukamilika kwa Mkutano huo wa amani, siku iliyofuata yaani Jumapili majira ya saa nne asubuhi mheshimiwa Amir Sahib Maulana Sheikh Chaudhry Sahib alianza safari yenye lengo la kwenda kufanya ziara mkoani Tabora. Kama ilivyo ada, hauwezi kutoka Mwanza na kwenda Tabora kwa barabara pasipo kupitia Shinyanga. Wanajumuiya wa Mkoa wa Mwanza (ambao ndio walikuwa walezi wa Mkoa wa Shinyanga kimahubiri na mengineyo) wakamuomba Amir Sahib apitie baadhi ya matawi mawili ya Shinyanga kabla ya kuelekea safari yake huko Tabora. Basi Amir sahib akaridhia na kukubali, ambapo alipita matawi ya Bugimbagu pale ambapo tulikuwa tumeanza Waqar e Amal (Ikiongozwa na wanajumuiya wa Mwanza) ya ujenzi wa msikiti na kuleta changamoto kadhaa kiujenzi, alifika na kufanyika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi na kufanya maombi kuelekea ujenzi huo wa msikiti. Siku hiyo nami muandishi wa Makala hii nilikuwa katika msafara huo kumsindikiza Amir Jamaat kutokea jijini Mwanza.

Nakumbuka tulikuwa na gari mbili huku mimi nikiendesha moja ya gari kumsindikiza Amir Sahib kutoka Mwanza na safari yangu ilikuwa ikiishia mkoani Shinyanga katika eneo la Nsalala. Tulipanga sisi baadhi ya wanajumuiya wa Mwanza basi tuishie mkoani Shinyanga, ili kuuruhusu msafara uelekee kirahisi mkoani Tabora kwani huko pia Mheshimiwa Amir Sahib alikuwa na ratiba za kikazi.

Tukiwa ndio tunaanza safari kutoka Mwanza, baadhi ya Waalimu ambao tayari walikuwa wameanza kuutumikia mkoa wa Shinyanga kwa wakati huo (Mwl Musa Kaswezi na Mwl Twaliat Zuberi) basi walifanya kuandaa mazingira ya kumpokea Amir Sahib ndani ya mkoa wa Shinyanga ili kuyatembelea matawi matatu pembezoni mwa mji wa Shinyanga, matawi hayo yalikuwa ni Negezi, Bugimbagu na pale mjini. Ikumbukwe wakati huo Jamaat ilikuwa imeanza (kwa udogo) kazi ya mahubiri, na harakati kadhaa za kupanua mahubiri nje ya Manispaa ya Shinyanga na kufika katika kijiji cha Nsalala, kijiji ambacho kipo katika barabara kuu itokayo Mwanza na kuelekea Dar es Salaam, kikiwa ni kijiji cha pili kutoka mpakani mwa Tabora na Shinyanga. Basi mimi na Bwn Yahya Kambaulaya tukajulishwa na waalim hao juu ya namna walivyopanga kumlaki na kumsalimu Amir Sahib akipita kuelekea mkoani Tabora, wakafanya maandalizi kumlaki Amir wa Jamaat pale kijijini Nsalala.

Ndugu zangu wapendwa na wasomaji, naomba ninukuu maandiko ya Masih Aliyeahidiwa[as] kama ifuatavyo:

i) I shall give you a large party of Islam – Nitakujaalia umma mpana/mkubwa katika Islam.

ii) Mimi nipo peke yangu na Allah yu pamoja nami, je mtu ambaye Mungu yupo upande wake anaweza kushindwa? - (Kitabu cha Ishara za Kimbingu)

Allahu Akbar! Mapokezi kijijini Nsalala ilikuwa ni mafuriko makubwa ya watu kumpokea Amir Sahib mwaka huo wa 2012, ilikuwa ni takriban kijiji kizima kilifurika na kukusanyika pamoja Nsalala. Kazi kubwa kabisa ilifanywa na Mwl Musa Kaswezi katika kuhakikisha kiongozi wetu mpendwa anapokelewa vema na kwa heshima zote pale Nsalala, na kuchagiza maendeleo makubwa ya mahubiri. Umati mkubwa sana ulifurika kuanzia pale barabarani Nsalala mpaka Shule ya msingi, ambapo ndio ilipangwa walau Amir Sahib asimame na kusalimiana na wanajamaat wachache na uma wa wanakijiji na kuwasilisha ujumbe wa Masih Aliyeahidiwa (as).

Hapo kijijini Nsalala Mheshimiwa Amir Jamaat alilakiwa na umati mkubwa sana wa wanajumuiya na wanakijiji waliojumuika kwa pamoja ili kumlaki mgeni wao. Alipofika tu hapo mheshimiwa Amir Jamaat alishuka kwa gari na kisha akasalimiana na ndugu wengi waliofurika kumpokea, na kuelekea eneo la shule ya msingi Nsalala ambapo hapo ndipo paliandaliwa eneo la kuketi kwa muda. Baada ya kuwasili eneo hilo la shule ya msingi, mheshimiwa Amir Sahib aliweza kuhutubu kwa muda mfupi kwa kuwashukuru ndugu wote waliofurika hapo kumlaki, na kisha hapohapo aliweza kutoa utambulisho wa Jumuiya ya Waislam Waahmadiya, na alimalizia kwa kuwaasa wananchi wote kujiepusha na matukio mabaya ya kuua vikongwe na albino. Alimaliza kwa maombi na kisha msafara wake kuelekea mkoani Tabora ulianza na hapo ndio tukamuaga rasmi kwa kuhitimisha ziara yake mkoani Shinyanga.

Ama kwa hakika, ujumbe wa Masih wa zama ukawasilishwa kupitia ujio wa ziara ya Amir sahib, mvuto mkubwa ukajiri kutoka kwa wanajumuiya wachache na wasiokuwa wanajumuiya. Mheshimiwa Amir Sahib akiwa hapo Nsalala njiani kwenda Tabora, akaendelea kufikisha ujumbe wa Amani juu ya mafundisho sahihi ya Islam Ahmadiyya huku akiwaasa jamii nzima kujiepusha na mauwaji ya vikongwe na walemavu wa ngozi. Alhamdulillah ujumbe ukapenya vema kwa jamii ya Wasukuma, nao wakapashana habari za tukio la ujio wa Amir Sahib kijiji baada ya kijiji juu ya kiongozi wa Islam amefika Nsalala na kuwafikishia ujumbe wa Dini Tukufu ya Islam na uwepo wa Mungu mmoja. Jamii pana ya wasukuma wakazidi kupashana ya kwamba, jamani hii ndio Dini ya kweli. Huyu kiongozi (mwarabu) ametufikia na ametuletea mafundisho mazuri sana. Ikawa gumzo kubwa kuanzia viunga vya vijiji vya Tinde, Nsalala yenyewe, Mwawaza, Shabuluba hadi kijiji cha Kidanda. Habari ikawa ni moja tu kuwa kuna Dini imekuja na mafundisho yake mazuri sana, na wakipashana kwa kisukuma kuwa (Dini yawiza sana – hii dini nzuri sana). Ikawa kila kijiji jirani wanapopata taarifa na habari juu ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, basi wanavijiji hao wakahitaji Jamaat iwafikie. Simu zikaanza kuwa nyingi kupokelewa, wengine wakiendesha baiskeli kutoka kijiji jirani na kufika kumtafuta Mwalimu kuwa “tunaomba na sisi mtufikie Kijijini kwetu” na ikaanza haja ya haraka sana kupata nguvu ya ziada ili kuwahudumia wale wanaojiunga na Jamaat na wapate malezi. Vichwa vikaanza kutuuma sisi wenyeji kwamba tutafanyaje tuweze kuwahudumia wanaojiunga na kuwapa **Tarbiyyat**, idadi ikawa inaongezeka kila uchwao. Ni katika tukio hili la Nsalala ndipo Mheshimiwa Amir Sahib alipoamua sasa ipo haja kubwa sana kuufanya mkoa huu kitovu cha mahubiri ya Jamaat nchini na kupanua mahubiri, na Mheshimiwa Amir Sahib Maulana Sheikh Tahir Chaudhry Sahib akatoa muongozo mwema na rasmi kutokea tawini Nsalala ikiwa ni mara yake ya kwanza kuuzuru mkoa wa Shinyanga, ili kuongeza sana bidii ya mahubiri mkoani humo. Hapa ndipo harakati kamilifu za chemchem ya mahubiri mkoani Shinyanga na ukanda wa Ziwa zilipoanzia.

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Mwongozo Mkuu, Manufaa na Fadhila

zisizo na Mwisho za Qur'ani Tukufu kwa Mtazamo wa Masihi Aliyeahidiwa[as]

Ufisadi umedhihirika barani na baharini.' (Qur'ani Tukufu 30:42). Ilikuwa ni wakati huu ambapo Qur'ani Tukufu iliteremshwa ambayo ilikanusha maovu yote na kurekebisha imani potofu za dini zilizotangulia. Haya yote yalifanyika kupitia kitabu cha kipekee na kilichokamilika, ambacho ni Qur'ani Tukufu. Hasa katika sura ya kwanza ya Qur'ani Tukufu, Mwenyezi Mungu alieleza kwa ukamilifu imani ya Uislamu na akakanusha uwongo wote wa dini zilizotangulia.

Muujiza Usio Kifani
Khalifa Mtukufu (atba) aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Qur'ani Tukufu ni muujiza. Muujiza unarejelea kitu kisicho cha kawaida ambacho hakiwezi kuigwa na mwingine yeyote awaye. Hiyo ndiyo Qur'ani Tukufu iliyowekwa mbele ya Arabia yote, na hakuna hata mmoja katika Arabia aliyeweza kuwasilisha kitu kama hicho. Huenda ilionekana kwao kuwa kitabu kama kitabu kingine chochote, lakini waligundua kuwa ilikuwa muujiza wakati hakuna mtu aliyeweza kuwasilisha kitu chochote kinachofanana nacho, na tangu wakati huo, hakuna mtu ambaye ameweza. Kwa hiyo, ni muujiza. Ni ishara inayoashiria uwepo wa Mungu kwa uhakika kabisa ambayo haiwezi kukanushwa au kukataliwa.
Imani nyingine zimewapeleka tu watu kufikia hatua ya kutambua kwamba panapaswa kuwepo Mungu. Mtu anaweza kutazama uumbaji wa ulimwengu na kufikia hitimisho kwamba lazima kuwe na Mungu. Mtu anaweza kuelewa kwamba kunapaswa kuwa na Mungu kupitia hoja zenye mantiki. Hata hivyo, hii hailingani na utambuzi halisi na uhakika wa ukweli kwamba Mungu kweli yupo. Ni kwa kuelewa tu na kutambua sifa za Mungu na kuona ishara Zake ambapo mtu hawezi tu kufikia uhakika wa kuwepo kwa Mungu, bali anaweza pia kupata uzoefu wa uwepo wa Mungu na kuanzisha uhusiano Naye yeye mwenyewe. Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba hiki ndicho kiwango tunachopaswa kujitahidi kukifikia; kutoegemea tu kwenye hoja zenye mantiki bali sisi wenyewe kutafuta na kuanzisha uhusiano na Mwenyezi Mungu kupitia ishara Zake.
Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba kuna mifano mingi ya hili kutokea ndani ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya. Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba kulikuwa na mtu kutoka Ubelgiji ambaye alimsimulia kwamba alikuwa mtu asiyeamini Mungu, hata hivyo, wakati yeye sio tu alielewa hoja za busara za kuwepo kwa Mungu, lakini pia aliona ishara zake na uzoefu wa Mungu yeye mwenyewe binafsi, aliachwa bila chaguo isipokuwa kukubali kuwako kwa Mungu.

Utimilifu wa Imani Kupitia Kitabu Kikamilifu
Khalifa Mtukufu (atba) zaidi alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alieleza kwamba Qur'ani Tukufu inasema:

Hicho ndicho Kitabu, kisicho na shaka yoyote ndani yake, ni mwongozo kwa wamchao (Allah). (Qur'ani Tukufu 2:3)
Kwa maneno mengine, Kitabu hiki kimeteremshwa kutokana na elimu ya Mwenyezi Mungu, na hivyo hakina shaka na dosari yoyote. Na kwa sababu ujuzi wa Mungu unaweza kumfikisha mwanadamu kwenye ukamilifu, ni mwongozo kwa watu wema. Watu wema ni wale wanaomwamini Mwenyezi Mungu kuwa ni Mjuzi wa ghaibu, na wanasimamisha Sala na wanatoa sadaka.
Khalifa Mtukufu (atba) aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Qur'ani Tukufu ilikamilisha imani, kama Mwenyezi Mungu anavyosema:

Leo Nimewakamilishieni dini yenu, na kuwatimizieni neema Yangu, na Nimewapendeleeni Islamu iwe dini yenu. (Qur'ani Tukufu 5:4)
Kwa hivyo, hakuna kitabu chochote kinachoweza kuchukuliwa kuwa bora kuliko Qur'ani Tukufu kwani baraka zinazopatikana kupitia Qur'ani Tukufu haziwezi kupatikana kwa chochote kingine. Khalifa Mtukufu (atba) alisema inasikitisha kwamba haya ni maoni yetu, lakini wapinzani wetu wanasema tumeivunjia heshima Qur'ani Tukufu.

Uponyaji wa Kiroho na Kuanzisha Mahusiano na Mwenyezi Mungu
Khalifa Mtukufu (atba) alimnukuu zaidi Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Qur'ani Tukufu ni chanzo cha uponyaji wa kiroho. Imejaa hekima ambayo imeainisha dini kamilifu na imeweka uponyaji wa kiroho sambamba na uponyaji wa kimwili.
Khalifa Mtukufu (atba) aliendelea kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba njia ya kweli ya kuanzisha uhusiano na Mwenyezi Mungu ni Qur'ani Tukufu. Mtu hawezi kuweka mafungamano Naye mpaka atambue dalili Zake na mpaka nuru Yake iingie kwenye moyo wake. Uhusiano huu unaweza kupatikana tu kwa kufuata yale ambayo yameainishwa ndani ya Qur'ani Tukufu. Hivyo, kwa kufuata mafundisho ya Qur'ani Tukufu, mtu anaweza kuuona uso wa kweli wa Mwenyezi Mungu. Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Waahmadiyya wanapaswa kuzingatia na kujichambua kama kweli wanafuata mafundisho ya Qur'ani Tukufu. Khalifa Mtukufu (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Amwezeshe kila mmoja wetu kufanya hivyo.
Khalifa Mtukufu (atba) alizidi kumnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba dalili zote mashuhuri zinazopaswa kuwepo katika maandiko matakatifu hazipo katika kitabu chochote isipokuwa Qur'ani Tukufu. Kati ya sifa kubwa bayana zinazopatikana katika Qur'ani Tukufu, moja ni kwamba inamchukua mtu kutoka kwenye hatua ya 'kuwe na Mungu' hadi 'Mungu hakika yupo'. Zaidi ya hayo, hakuna anayeweza kuiga ishara zilizowasilishwa na Mwenyezi Mungu katika Qur'ani Tukufu. Hata kama watu wangekusanyika pamoja kujaribu kuiga au kuibua ishara hawataweza kupata kitu chochote ambacho kinasimama popote karibu na dalili za Qur'ani Tukufu. Ni Qur'ani Tukufu pekee inayodhihirisha uwezo wa Mwenyezi Mungu. Na kwa wale wanaoifuata Qur'ani Tukufu, Mwenyezi Mungu anaahidi:

'... habari njema ni kwao; basi wape habari njema watumishi Wangu.' (Qur'ani Tukufu 39:18)
Na Mwenyezi Mungu pia aliahidi katika Qur'ani Tukufu:

... na Akawasaidia kwa Roho itokayo Kwake. (Qur'ani Tukufu, 58:23).
Na Mwenyezi Mungu Anaahidi:

Enyi mlioamini, mkimcha Allah Atawafanyieni alama ipambanuayo na Atawafutieni makosa yenu na kuwasameheni; na Allah ni Mwenye fadhili kuu. (Qur'ani Tukufu, 8:30).
Masihi Aliyeahidiwa (as) alisema kwamba yeye mwenyewe ni shahidi na anazishuhudia ishara hizi, na Masihi Aliyeahidiwa (as) alitumwa ili kutusaidia kuzitambua.

Kumpata Mwenyezi Mungu katika Maneno ya Qur'ani Tukufu
Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba Masihi Aliyeahidiwa (as) alieleza kwamba hadithi na simulizi zinazopatikana ndani ya Qur'ani Tukufu kwa hakika ni bishara. Qur'ani Tukufu ni mkondo wa haki na bahari ya bishara. Haiwezekani kwa mtu kufikia yakini juu ya Mwenyezi Mungu bila ya Qur'ani Tukufu. Mungu aliyefichwa kwa ulimwengu anaweza kutambuliwa na kupatikana kupitia Qur'ani Tukufu.
Khalifa Mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) kwamba zote mbili amri na hadithi au masimulizi yanapatikana ndani ya Qur'ani Tukufu. Wale ambao hawawezi kutofautisha kati ya hizo mbili wanajikuta katika shida kubwa. Wanabakia bila kufaidika na Qur'ani Tukufu. Imeelezwa katika Qur'ani Tukufu:

Je, hawaitafakari Qur'an? Na kama ingalitoka kwa asiyekuwa Allah, bila shaka wangalikuta ndani yake hitilafu nyingi. (Qur'ani Tukufu 4:83).
Ukweli kwamba hakuna mgongano katika Qur'ani Tukufu ni dalili ya ukweli wa Qur'ani Tukufu.

Ubora wa Kurani Juu ya Maandiko Mengine
Khalifa Mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alieleza kwamba mafundisho ya Qur'ani Tukufu ni bora kuliko mafundisho mengine yoyote. Torati inafundisha jicho kwa jicho, Injili inafundisha kugeuza shavu jingine, hata hivyo Qur'ani Tukufu inatoa mafundisho yenye uwiano na manufaa kabisa ya:

Na malipo ya ubaya ni ubaya ulio sawa nao; lakini anayesamehe kwa nia ya kusuluhisha, basi ujira wake ni juu ya Allah … (Qur'ani Tukufu, 42:41).

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba mada hii itaendelea kwa kuzingatia nukuu za Masihi Aliyeahidiwa (as) katika siku zijazo.
Khalifa Mtukufu (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Atuwezeshe kutekeleza kwa ukweli mafundisho ya Qur'ani Tukufu.

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

MapenziyaMungu

SHABAN-RAMAZAN.1444AH | MACHI 2023 | ZAHOOR 1402 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufusaw

Abu Huraira^ra anasimulia kwamba: Nilimsikia Mtume^saw akisema: Abu Huraira wallahi mimi naomba msamaha kwa Allah kutubia kwake kwa siku moja zaidi ya mara sabini (**Bukhari**).

Mwongozo Mkuu, Manufaa na Fadhila

zisizo na Mwisho za Qur'ani Tukufu kwa Mtazamo wa Masihi Aliyeahidiwa^as

Kwa Jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu

Ubora wa Qur'ani Tukufu - Mafundisho ya Juu Zaidi

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah al-Fatiha, Khalifa mtukufu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (aba) alisema kwamba katika hotuba ya Ijumaa iliyopita, aliwasilisha nukuu mbalimbali za Masihi Aliyeahidiwa (as) kuhusu ubora na uzuri wa Qur'an tukufu.
Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba atawasilisha nukuu zaidi leo.
Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba katika kitabu chake Tohfa-e-Qaisariyyah (Zawadi kwa Kaisari) ambacho Masihi Aliyeahidiwa (as) aliandika ili kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa Malkia Victoria katika Jubilee yake ya Almasi, alisema kwamba Qur'ani Tukufu imejaa hekima ya kina na ni bora kuliko Injili katika kuzalisha utawa. Mungu wa Kweli anaweza kushuhudiwa kupitia Qur'ani Tukufu tu. Qur'ani Tukufu iliurejesha umoja wa Mungu ambao ulipotea duniani. Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba ni nani mwingine ambaye angeweza kufikisha ujumbe wa Uislamu kwa mfalme kwa imani kama hiyo isipokuwa Masihi Aliyeahidiwa (as)?



Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa Tanoatba akihutubia waaminio Ijumaa katika Masjid Mubarak, Uingereza Tarehe 10 Februari, 2023. Akieleza Mwongozo Mkuu, Manufaa na Fadhila zisizo na Mwisho za Qur'ani Tukufu kwa Mtazamo wa Masihi Aliyeahidiwa^as

Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba pamoja na ukweli huu, Waislamu wasiokuwa Waahmadiyya bado wanathubutu kusema kwamba Waahmadiyya wanaivunjia heshima Qur'ani Tukufu. Zaidi ya hayo, watu wasiokuwa Waislamu wanapotambua kwamba hawawezi kushindana au kuikanusha Qur'ani Tukufu, wanakimbilia kufanya mambo kama vile kuichoma moto Qur'ani Tukufu, kama ilivyoonekana hivi karibuni huko Sweden na imeonekana huko nyuma katika nchi zingine za Skandinavia. Khalifa Mtukufu (atba) alisema kwamba kama Waislamu wote wangeungana chini ya bendera ya Masihi Aliyeahidiwa (as), basi hakuna yeyote ambaye angethubutu kufanya vitendo viovu kama vile kuchoma Qur'ani Tukufu.
Mwongozo Kamili wa Kuwatoa Wanadamu Katika Giza
Khalifa Mtukufu (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Qur'ani Tukufu imewasilisha elimu kamili na mwongozo kamili kwa ajili ya matendo gani yanapaswa kutekelezwa. Inatufundisha 'Tuongoze kwenye njia iliyonyooka' ili tuweze kunufaika na elimu kamili ya Qur'ani Tukufu na kisha inatufundisha 'Njia ya wale ambao umewaneemesha' ili tuweze kuikanyaga njia iliyokamilika, njia ya mwongozo iliyoainishwa na Qur'ani Tukufu. Kutenda kulingana na mafundisho ya Qur'ani Tukufu kuna faida inayoonekana ambapo mtu hujikurubisha kwa Mwenyezi Mungu na kuongezeka kwenye wema.
Khalifa Mtukufu (atba) zaidi alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba Qur'ani Tukufu iliteremshwa katika wakati ambapo ulimwengu ulikuwa umezama katika ufisadi na machafuko yalikuwa yameenea. Qur'ani Tukufu yenyewe inaielezea kama:

Endelea uk.11



HAJA YA IMAMU

Tafsiri ya Kitabu kwa Kiswahili,
Zaruratul-Imam

Hazrat Mirza Ghulam Ahmad^as (18351908◎), Mwanzilishi mtakatifu wa Jama'at Ahmadiyya Duniani, mzaliwa wa Qadian, katika kijiji cha Punjab, India, kilikuwa cha kimungu aliyeteuliwa kuwa Mwanamatengenezo wa Siku za Mwisho na Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi. Alitumwa na Allah kwa utimilifu wa unabii uliomo katika Biblia Takatifu, Quran Tukufu na Hadith, na kazi ya wazi ya kuugundua Uislamu tena usafi wake wa siku za nyuma na uzuri, na kuleta wanadamu wamrudie Muumba.

Zaruratul-Imam, au hitaji la Imamu, inaelezea kwa kina uharaka na hitaji la Imam wa zama, na sifa zake na alama kuu kama mwongozo uliowekwa na Mungu, sauti kueleza ya umri, na mara kwa mara mpokeaji wa Aya za Mwenyezi Mungu, na jinsi zote sifa hizi zipo kimilifu ndani ya mtu wa Mwandishi Mtakatifu.

Nakala hii itapatikana kwa bei ya Sh. 2,900/=

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie
mapenziyamungu36@gmail.com